

TUME YA PAMOJA YA FEDHA

KAZI ZA MSINGI ZA TUME ZINAZOTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/18

I Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Tume ya Pamoja ya Fedha imepanga kukamilisha kazi zifuatazo:-

a) Stadi ya Uwekezaji katika Mambo ya Muungano

Stadi ya Uwekezaji katika Mambo ya Muungano inalenga kuainisha na kuchambua Makampuni na Mashirika ya Muungano kuhusu Usimamizi na Uendeshaji wake na kutoa mapendekezo yatakayoimarisha ushiriki wa pande mbili za Muungano.

b) Mapitio ya Stadi ya Uchambuzi wa Kubainisha Wizara na Asasi za Muungano na Gharama za kuendesha Mambo ya Muungano na Stadi ya Mfumo Bora wa Kodi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mapitio ya Stadi hizi yanalenga kuhuisha takwimu na taarifa zilizotumika kwenye stadi hizo, pamoja na kuboresha mapendekezo yaliyotolewa ili yaendane na wakati na mabadiliko ya miundo ya kiasasi na sera.

II Katika Mwaka wa Fedha, 2017/18 Tume, inafanya mapitio ya:

Mapendekezo ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 133, kutakuwepo na Akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa ajili ya kuweka fedha zitakazotumika kuendesha Mambo ya Muungano. Tume ya Pamoja ya Fedha inafanya mapitio ya Mapendekezo ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja yanayolenga katika kuhuisha takwimu na taarifa zilizotumika kwenye kuandaa mapendekezo ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja, ili ziendane na wakati, kwa kuzingatia mabadiliko ya muundo wa Wizara na Asasi, pamoja na kufanyia marejeo mapendekezo yaliyotolewa.

III Aidha, Tume inaendelea kufanya uchambuzi wa Takwimu za Mapato na Matumizi ya Muungano kwa lengo la kuwa na kanzidata ya taarifa za fedha zinazohusu Mambo ya Muungano.